OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

27/04/2017

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inakaribisha maombi toka kwa Makampuni na Watu binafsi wenye sifa stahiki na uwezo kisheria kufanya kazi ya Huduma ya Uwakala wa ukusanyaji Mapato ya vyanzo vifuatavyo;-

A: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/01: USHURU WA MINADA

Ushuru huo utakusanywa katika Minada ya Basodesh tarehe 4 ya kila mwezi, Hirbadaw tarehe 5 ya kila mwezi, Bassotu tarehe 6 ya kila mwezi, Gawidu tarehe 7 ya kila mwezi, Ishponga tarehe 8 ya kila mwezi, Gehandu tarehe 9 ya kila mwezi, Katesh terehe 10 na 27 ya kila mwezi, Gisambalang tarehe 11 ya kila mwezi, Simbay tarehe 12 ya kila mwezi, Endasaki tarehe 13 na 29 ya kila mwezi na Dirma tarehe 28 ya kila mwezi.

B: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/02: USHURU WA MAZAO YA CHAKULA

Ushuru huo utakusanywa katika Vituo vyote vya Tarafa za Katesh, Endasak, Bassotu, Balangdalalu na Simbay **isipokuwa Ushuru wa Mashamba makubwa ya Bassotu Plantation, Mulbadaw, Murjanda, Gidagamowd, Setchet na Gawal utakusanywa na Halmashauri yetu.**

C: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/03: USHURU WA MAZAO YA MALIASILI NA MISITU

Ushuru huo utakusanywa katika Vituo vyote vya Tarafa za Katesh, Endasak, Bassotu, Balangdalalu na Simbay

D: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/04 :USHURU WA KITUO CHA MABASI KATESH/STENDI YA MABASI KATESH

Ushuru huo utakusanywa katika Kituo cha Mabasi Katesh/Stendi ya Mabasi Katesh

E: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/05 :USHURU WA HUDUMA YA CHOO CHA STENDI YA KATESH

Ushuru huo utakusanywa katika cha Choo cha Stendi ya Katesh.

F: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/06: ADA YA USAFI WA MAZINGIRA KATIKA MJI WA KATESH

Ada hiyo itakusanywa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katesh.

G: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/07: HUDUMA YA UKODISHAJI WA KANTINI YA HALMASHAURI

Kantini hiyo itakodishwa kwa Mtoa Huduma atakayetoa Huduma ya Chakula kwa Watumishi wa Halmashauri na watu mbalimbali watakaohitaji huduma hiyo.

H: ZABUNI NA LGA/059/HQ/2017/2018/NC/08: USHURU WA MALI GHAFI ZA UJENZI KATESH

Ushuru huo utakusanywa kutokana na uchimbaji wa kokoto,mchanga na mawe katika eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katesh.

Kipindi cha kuanza kukusanya Mapato hayo ni Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kuanzia tarehe 01/07/2017 hadi tarehe 30/06/2018.

Waombaji wanaweza kununua Kabrasha la Zabuni (Tender Document) kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri baada ya kulipa ada ya maombi ya Tsh 50,000/= ambayo haitarudishwa. Fedha hizo zitalipwa Benki baada ya Muombaji wa Zabuni kuchukua "Bill" kutoka kwa Mhasibu wa mapato ya Halmashauri ya Wilaya siku za kazi Jumatatu-Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi 9:30 Alasiri .

- Muombaji wa Zabuni atakayeshinda zabuni atalazimika kutumia mashine ya Kieletroniki "Point Of Sale" (POS) na ataweka fedha zote katika akaunti ya Halmashauri na yeye atarudishiwa asilimia yake ya "Commission"

- Muombaji asiwe Diwani wala Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang
- Muombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kuweka Dhamana ya kiwango cha chini cha fedha za asilimia za mwezi mmoja ambazo amekubaliwa kabla hajaanza kukusanya mapato.
- Muombaji wa zabuni anaweza kutembelea maeneo ya Ukusanyaji mapato kwa gharama zake ili aweze kuaandaa makisio ya takwimu zake kabla ya kujaza zabuni .

BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATANISHWE NA MAELEZO KAMILI NA VIVULI (vilivyothibitishwa) vifuatavyo:

1. Leseni (halali) ya Biashara husika.
2. Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni.
3. Stakabadhi ya Ada ya Maombi ya Zabuni ya Shilingi Elfu Hamsini tu (50,000/=) isiyorudishwa
4. Maelezo ya kazi ilizowahi kufanya na uzoefu usiopungua miaka miwili wa huduma ya Uwakala wa ukusanyaji Mapato na Vielelezo vilivyothibitishwa na Waajiri wa awali kwa kazi husika.
5. Usajili wa TIN.
6. Usajili wa VAT (Kama inahusika).
7. Uthibitisho wa ulipaji Kodi (Tax Clearence Certificate) ya mwaka 2017
8. Muombaji ataje kiasi Asilimia ya "Commission" atakayolipwa na Halmashauri ya wilaya kutokana na Mchanganuo wake.
9. Muombaji aonyeshe idadi ya wafanyakazi /Watendaji wake pamoja na sifa za Kitaaluma, Uzoefu/Ujuzi na Maadili ya kazi ya Huduma ya Ukusanyaji Mapato (Uthibitisho unahitajika).
10. Muombaji ataje Nyenzo za Usafiri anazomiliki au atakazotumia (aonyeshe uhali wa Umiliki au Mkataba wa kukodi uliothibitishwa).

11. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyoidhinishwa na kuthibitishwa na Meneja na Tawi la Benki husika.

12. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of Attorney) wa mtu atakayehusika na Zabuni hii.

13. Muombaji aoneshe Taarifa za Hesabu za Kampuni za miaka miwili (2) hadi mitatu (3) iliyomalizika kabla ya kuomba Zabuni hii zilizokaguliwa na kuthibitishwa na Mkaguzi wa Hesabu (aliyethibitishwa – Certified Public Accountant/Auditor).

14. Taarifa ya madeni yake yote (kama yapo) anayodaiwa na watu binafsi, Benki au Taasisi nyingine

15. Mzabuni anaweza kuomba zaidi ya Chanzo kimoja.

    (i) Zabuni itakayowasilishwa bila kukamilika itaondolewa katika hatua za awali.

    (ii) Tathmini na tuzo itatolewa kwa Mzabuni kwa kuzingatia chanzo kimoja alichoshinda au mchanganyiko wa Vyanzo.

16. Maombi yote ya Zabuni yakiwa yamefungwa kwenye Bahasha yatumwe kwa;-

    KATIBU WA BODI
    BODI YA ZABUNI
    HALMASHAURI YA WILWAYA YA HANANG
    S.L.P 2 KATESH-HANANG

17. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 19/05/2017 saa 5:00 asubuhi katika Ukumbi wa Halmashauri Block "D" na Zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho.
18. Maombi ambayo hayatapokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubaliwa
19. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa siku ya ufunguzi

EDWIN MWAMPAMBA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HANANG.